(vii) Kwanini mazingira machafu ni mabaya kwa afya?

A. Husababisha ulemavu  C. Husababisha umaskini
B. Husababisha uzembe  D. Husababisha magonjwa [   ]

(viii) Kazi ipi ya ninadamu husababisha uchafuzi wa hewa?

A. Viwanda  B. Utalii  C. Biashara  D. Uvuvi [   ]

2. Oanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika **Fungu A** na aina ya shughuli za kiuchumi katika **Fungu B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

<table>
<tr><th>No.</th><th>Fungu A</th><th>Herufi</th><th>Fungu B</th></tr>
<tr><td>(i)</td><td>Kukosekana kwa malisho mazuri</td><td></td><td rowspan="6">A. Kilimo<br>B. Misitu<br>C. Uchimbaji wa madini<br>D. Ufugaji wa ndege<br>E. Ufugaji wa wanyama<br>F. Utalii<br>G. Uvuvi<br>H. Uwinndaji</td></tr>
<tr><td>(ii)</td><td>Kupungua kwa samaki kutokana na matumizi ya sumu na nyavu zenye matundu madogo.</td><td>[   ]</td></tr>
<tr><td>(iii)</td><td>Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa katika migodi</td><td>[   ]</td></tr>
<tr><td>(iv)</td><td>Matangazo duni ya kuvutia wageni kuja kuangalia urithi wa asili na mbuga za wanyama</td><td>[   ]</td></tr>
<tr><td>(v)</td><td>Utengenezaji wa mkaa na kukata miti ovyo</td><td>[   ]</td></tr>
<tr><td>(vi)</td><td>Kupungua kwa chakula kutokana na upungufu wa mvua na udongo kukosa rutuba.</td><td></td></tr>
</table>

## SEHEMU B (Alama 22)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Ujima ulikuwa mfumo wa kwanza wa kiuchumi ambao binadamu wote waliupitia. Hapakuwa na unyonyaji miongoni mwa watu kwa kuwa kila mmoja alishiriki katika uzalishaji. Katika mfumo huu, njia kuu za uzalishaji mali zilikuwa ardhi, misitu, maziwa na mito. Wakati wa ujima, uzalshaji mali ulikuwa mdogo sana. Hii ilitokana na vitendea kazi duni vilivyotumika. Vilevile hapakuwa na biashara wala kubadilishana bidhaa baina ya watu katika jamii. Hii ilitokana na kukosekana kwa ziada wakati wa kuzalisha. Mfano wa vitendea kazi vilivyotumika ni majembe ya mkono na mishale. Katika kipindi cha ujima, njia za uzalishaji mali na vitendea kazi vilimilikiwa na jamii nzima.

### Maswali:


(i) Bainisha njia mojawapo kuu ya uzalishaji mali wakati wa ujima.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) Kifaa gani kilitumika katika kuwinda?
(iii) Kwa nini hapakuwa na unyonyaji katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
(iv) Kwanini hapakuwa na biashara katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
(v) Nani alifaidika kutokana na mali zilizozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
(vi) Kwanini hapakuwa na mazao ya ziada yaliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali?
(vii) Ni kwa jinsi gani njia za uzalishaji mali zilimilikiwa?

4. Soma ramani ya Kijiji cha Lumbila kisha jibu kipengele cha (i) – (iv) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.




(i) Kuna shule ngapi katika kijiji cha Lumbila? ________________
(ii) Kanisa lipo upande gani toka daraja lililo karibu? ____________
(iii) Kuna milima mingapi katika kijiji cha Lumbila? ______________
(iv) Ni barabara ngapi zinaelekea Kaskazini mwa Kijiji cha Lumbila?


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org